

KISU CHANGU

1. Sichinjii kisu changu, vinyama vidogodogo.
Sungura na nungunugu, na paa kwenye mitego.
Vifavyo kwa moja rungu, teke moja kwao pigo.
Vinyama vidogodogo, sichinjii kisu changu.
2. Sichinjii katakata, vinyama vilavyo ndago.
Vichimbuavyo matuta, pembe za nyumba kwa zogo.
Viazi vinatafuta, na vizizi vya mihogo.
Vinyama vidogodogo, sichinjii kisu changu.
3. Sichinjii naapia, kwa fimbo au kigogo.
Vipigwapo hujifia, kama dagaa wa dago.
Kisu changu kutumia, nite jina la udogo.
Vinyama vidogodogo, sichinjii kisu changu.
4. Sichinjii asikhofu, ndege penye lake tago.
Shingo yake siyo kufu, ni nyembamba kisha ndogo.
Sikitii usumbufu, ndege hawapa kichogo.
Vinyama vidogodogo, sichinjii kisu changu.
5. Sichinjii ila twiga, kongoni pofu na mbogo.
Hazengeya kwenye mbuga, hawindia mtatago.
Hachinja n'kisha piga, kwa pigo la kwenye kogo.
Vinyama vidogodogo, sichinjii kisu changu.
6. Sichinjii chaparara, nachinja wenye mnogo.
Wenye kiga na sarasara, wa nundu na nono figo.
Nyama zitiazoo fora, mapande fungu mzigo.
Vinyama vidogodogo, sichinjii kisu changu.
7. Sichinjii bora nile, hata zife kwa marogo.
Njaa taipa simile, ingasaga kwa misago.
Nasubiri wenda mbele, fisi nyuma chegochego.
Wanyama wadogodogo, sichinjii kisu changu.
8. Sichinjii walodhuli, hapa naweka kiago.
Nachinja wenye miili, wa pori au mifugo.
Nyama mapande mawili, hukinaisha magego.
Kamwe vinyama vidogo, sichinjii kisu changu.

Amiri A.S. Andanenga (Sauti ya Kiza)
Kinondoni-Shamba
DAR ES SALAAM